Kijarida Kuhusu

Ushahidi

Kimeandaliwa na:

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

© LHRC

Septemba, 2013

Yaliyomo

SHUKURANI.....v

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU.....v

MAONO.....v

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI.....v

LENGO KUU.....vi

DIBAJI.....vii

1.0 UTANGULIZI.....1

2.0 TAFSIRI/MAANA YA USHAHIDI.....1

2.1 Aina za Ushahidi..... 1

2.1.1 Ushahidi wa Matamshi.....1

2.1.2 Ushahidi wa Maandishi.....2

2.1.3 Ushahidi wa Uhalisi.....2

2.1.4 Ushahidi wa Kimazingira.....3

3.0 KUTHIBITISHA TUHUMA, MASHITAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI.....3

4.0 KUKANUSHA TUHUMA, MASHITAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI..... 3

5.0 AINA ZA MASHAHIDI..... 4
5.1 Shahidi ni Nani?..... 4
5.2 Nani Anaweza kuwa Shahidi?..... 4
5.3 Mume na Mke..... 5
5.4 Shahidi wa utaalamu maalum au fani... 5
5.5 Mtu mwenye Matatizo ya Akili (Mwenye Mtindio wa Ubongo)..... 6

6.0 KUHOJI NA KUULIZA MASWALI MASHAHIDI..... 6
6.1 Upande wa Mashitaka au Mlalamikaji. 6
6.2 Upande wa Utetezi au Mdaiwa..... 7
6.3 Mahakama..... 7

7.0 KUPOKELEWA NA KUKUBALIWA KWA USHAHIDI MAHAKAMANI..... 7

8.0 HITIMISHO..... 8

SHUKURANI

Tunatoa shukurani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa vijarida hivi. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la tatu hususan Wakili Harold Sungusia, Wakili Fulgence Massawe, Wakili Jeremiah Mtobesya, Bw. Rodrick Maro na Bw. Evans Sichalwe, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria za Tanzania mnamo Septemba, 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina tamani jamii yenye haki na usawa.

TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa utakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa sheria.

DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta

katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama angejua sheria. Ndio maana basi Kituo kimeamua kutoa machapisho haya na mengine, kwa lengo la kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelekezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika vijitabu hivi tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapopata matatizo ya namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia. Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali umsaidie na mwenzako kupata usaidizi huu.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

1.0 UTANGULIZI

Masuala yanayohusu ushahidi nchini yanasimamiwa na Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 ya Sheria za Tanzania, ya mwaka 1967. Sheria hii inaweka masharti ya jumla ya sheria ya ushahidi nchini Tanzania japo sheria nyingine zinaweza pia kuweka vipengele maalum kuhusiana na mazingira na mahitaji maalum ya sheria husika.

2.0 TAFSIRI/MAANA YA USHAHIDI

Ushahidi ni njia ambayo hutumika kuthibitisha au kukanusha masuala au tuhuma iliyopo au jambo linalobishaniwa.

2.1 Aina za Ushahidi

Kuna aina kuu nne za ushahidi nazo ni:-

1. Ushahidi wa matamshi;
2. Ushahidi wa maandishi;
3. Ushahidi wa uhalisia; na
4. Ushahidi wa kimazingira.

2.1.1 Ushahidi wa Matamshi

Huu ni ushahidi usio wa maandishi ambao unatolewa moja kwa moja kwa mdomo wa shahidi. Misingi ya kukubalika ushahidi huu ni kama ifuatavyo:-

(a) Iwapo unahusisha suala la kuona, ushahidi huo unatolewa na shahidi aliyeshuhudia kuona

kitendo hicho;

(b) Iwapo unahusisha kusikia, ni lazima utolewe na shahidi aliyesikia;

(c) Iwapo unahusisha hisia nyinginezo tofauti na kusikia pamoja na kuona ni lazima ushahidi huo utolewe na shahidi aliyepata hisia hizo mfano, kuguswa, kuonja au kunusa.

2.1.2 Ushahidi wa Maandishi

Ushahidi wa maandishi ni ushahidi wowote unaotolewa kwa maandishi mahakamani. Ushahidi huu unaweza kuwa katika nyaraka, picha, alama yoyote, kanda ya video au radio au katika hali yoyote, ambayo ni imara, ya kudumu na kusomeka au kutambulika.

Ushahidi wa maandishi unatakiwa uwe katika hali ya asilia isipokuwa pale sheria inaporuhusu unaweza kutolewa kwa nakala.

2.1.3 Ushahidi wa Uhalisi

Ushahidi wa uhalisia, ni ushahidi ule ambao unatolewa kwa kuonyesha kitu, mfano kisu kilichotumika kuulia, au mikanda ya video, au picha, au kutembelea eneo la tukio mfano pale panapotokea mgogoro wa shamba.

2.1.4 Ushahidi wa Kimazingira

Ushahidi wa kimazingira, ni ushahidi unaopatikana baada ya kuunganisha matukio sehemu tukio lilipotokea na maelezo yanayotoa tafsiri ya mazingira maalum yanayothibitisha jambo au tukio.

3.0 KUTHIBITISHATUHUMA,MASHITAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI

Mtu yeyote ambaye anashitaki, amefungua shauri, anaiomba au kuitaka mahakama itoe uamuzi au hukumu katika mashitaka au shauri kwa manufaa yake analazimika kuwasilisha mahakamani ushahidi unaojenga hoja kuthibitisha madai au tuhuma anazozitoa dhidi ya mtuhumiwa, mshitakiwa au mdaiwa. Kiwango cha uthibitishaji wa tuhuma, dai au hoja katika kesi ya jinai ni kutoacha shaka yoyote, na katika kesi ya daawa ni ukweli kwa kiwango kikubwa au cha kusadikika.

4.0 KUKANUSHA TUHUMA, MASHITAKA, SHAURI AU USHAHIDI MAHAKAMANI

Niwajibu wa mtu yeyote ambaye anatuhumiwa, anashitakiwa au ushahidi umetolewa dhidi yake katika shauri kujitetea, kukanusha tuhuma, shitaka au ushahidi uliotolewa dhidi yake kwani asipofanya hivyo mahakama inaweza kutoa uamuzi dhidi yake.

5.0 AINA ZA MASHAHIDI

5.1 Shahidi ni Nani?

Shahidi ni mtu yeyote ambaye anatoa maelezo kuthibitisha tuhuma, shitaka au tukio fulani mbele ya Mahakama.

5.2 Nani Anaweza kuwa Shahidi?

Kutokana na sheria ya ushahidi ya mwaka 1967, watu wote wanaweza kuwa mashahidi isipokuwa pale mahakama inapoona kuwa hawaelewi kile wanachokisema au kuulizwa na pia hawatoi majibu ya kueleweka labda kwa sababu ya umri mdogo, uzee, magonjwa au kitu kingine chochote.

Mfano mtoto mdogo wa chini ya umri wa miaka (14) anaweza kutoa ushahidi juu ya jambo fulani na ushahidi wake unapokelewa kwa kiapo ikiwa mtoto huyo ataonekana kuelewa maana ya kiapo. Ikiwa mahakama itaona mtoto haelewi maana ya kiapo, ushahidi wake utachukuliwa kwa kuangalia kuwa mtoto ni muelewa na anaelewa kwamba anatakiwa kuongea ukweli mtupu mbele ya mahakama.

Kwa kawaida mahakama inatakiwa kujitahadharisha yenyewe wakati inapopokea na kutumia ushahidi wa mtoto.

5.3 Mume na Mke

Sheria inaeleza kuwa mume au mke ni mashahidi ambao wanaweza kutoa ushahidi lakini hawawezi kulazimishwa kutoa ushahidi dhidi ya mwenzi wake isipokuwa kwenye mashitaka yanayohusu makosa ya kujamiiana na yaliyo kwenye sheria ya ndoa au kosa analoshitakiwa nalo linamhusu mke, mume au mtoto au mali zao.

Mwendesha mashitaka anapotaka kumuita mume au mke kama shahidi wake kwa namna yoyote ile mfano, kwa maandishi au kutoa ishara mradi ushahidi wake utaeleweka na ni lazima ushahidi huu utolewe katika mahakama ya wazi. Ushahidi wa aina hii unachukuliwa kama ushahidi wa matamshi.

5.4 Shahidi wa utaalamu maalum au fani

Ushahidi wa mtaalamu juu ya jambo fulani pia hukubalika. Mfano daktari anaweza kutoa ushahidi kuhusu sababu ya kifo cha mtu ambaye alimtibu au kufanya uchunguzi wa sababu ya kifo chake.

Muhimu

Mahakama haifungwi na ushahidi wa utaalamu maalum au fani bali inaupima kama ushahidi mwingine na inaweza kuukataa au kutouzingatia katika kutoa maamuzi yake.

5.5 Mtu mwenye Matatizo ya Akili (Mwenye Mtindio wa Ubongo)

Mtu mwenye matatizo ya akili anaweza kutoa ushahidi kwa kitu anachokielewa isipokuwa pale mahakama itakapoona kwamba haelewi anachosema au kuulizwa na hivyo ushahidi wake kutokuaminika na hajui maana ya kiapo.

6.0 KUHOJI NA KUULIZA MASWALI MASHAHIDI

Shahidi anayetoa ushahidi mbele ya mahakama anaulizwa maswali na pande tatu;

(i) Upande wa mashitaka, mdai au mlalamikaji anaouunga mkono katika ushahidi;

(ii) Upande wa utetezi, mlalamikiwa au mdaiwa;

(iii) Mahakama.

6.1 Upande wa Mashitaka au Mlalamikaji

Mtu yoyote ambaye analalamika au kushitaki, ana haki ya kuita mashahidi ambao atawauliza maswali kwa lengo la kuthibitisha madai au mashitaka yake. Hawa mashahidi wanatakiwa kuunga mkono yale anayoyasema/anayolalamikia ili kuweza kuyathibitisha na hivyo kuweza kujenga kesi au shauri lake hatimaye kushinda.

Maswali anayotakiwa kuwauliza mashahidi wake yasiwe ya kuwaongoza shahidi bali ya kuwawezesha kueleza ukweli wanaofahamu kuhusu jambo linalobishaniwa. Upande wa mdaiwa au mshitakiwa una haki ya kuwauliza maswali mashahidi wa upande wa utetezi

kwa lengo la kudhoofisha, kanusha au kupima ukweli na uzito wa ushahidi uliotolewa na mdai au mshitaki.

6.2 Upande wa Utetezi au Mdaiwa

Upande wa utetezi una haki ya kuita mashahidi wake na kuwauliza maswali kwa lengo la kujenga utetezi wake. Maswali hayo yasiwe ya kumuongoza shahidi kusema ambayo mdaiwa anataka aseme. Ushahidi uwe ni wa kujenga kesi ya utetezi kwa kueleza ukweli unaomwondolea mdaiwa au mshitakiwa hatia au lawama.

Vile vile upande wa mdai au mshitaki una haki ya kuuliza maswali mashahidi wa mdaiwa au mshitakiwa wa mashitaka kwa lengo la kukanusha, kudhoofisha au kupima ukweli na uzito wa ushahidi uliotolewa na upande wa mdaiwa au mshitakiwa.

6.3 Mahakama

Mahakama ina haki ya kuuliza maswali pande zote katika shitaka au shauri ili kupata ufafanuzi au ukweli wa jambo linalobishaniwa.

7.0 KUPOKELEWA NA KUKUBALIWA KWA USHAHIDI MAHAKAMANI

Mahakama ndiyo yenye mamlaka ya kukubali au kukataa kupokea shahidi. Mahakama inafanya hivyo kwa kuzingatia kanuni za kutolewa kwa ushahidi huo na kama unahusu suala linalobishaniwa.

8.0 HITIMISHO

Ni muhimu kuzingatia na kufuata kanuni za kutoa ushahidi ili ukubalike mahakamani kwa ajili ya kukanusha au kuthibitisha jambo linalobishaniwa ili mtu aweze kupata haki yake.

Mashahidi wa upande mmoja, mfano mdai, mashitaka au mlalamikaji wanatakiwa kutoa ushahidi unaoshabihiana ambao haupingani ili kuweza kuthibitisha jambo linalobishaniwa, vilevile kwa upande wa utetezi.

Idadi ya mashahidi si hoja bali kinachotakiwa ni ukweli, uzito na kushabihiana kwa ushahidi unaotolewa. Hivyo shahidi mmoja anaweza kuwa na ushahidi mzuri na kuthibitisha jambo linalobishaniwa vizuri zaidi kuliko mashahidi wengi ambao hawajui wayasemayo na ushahidi wao unapingana au hauna mtiririko.

Hivyo kabla mtu hajafungua shauri au mashitaka mahakamani, lazima ajiulize kama ana ushahidi wa kutosha au kabla hajajitetea au kukanusha mashitaka, tuhuma au madai lazima ajiulize kama ana ushahidi.

Ndugu msomaji, umepata elimu ya kutosha kuhusu ushahidi, pamoja na kanuni za kutoa ushahidi mahakamani. Ni ombi letu kuwa elimu hii uliyoipata usikae nayo mwenyewe uitoe kwa jamii nzima ili tuwe na jamii ya ufahamu wa kutosha kuhusu sheria za nchi.